
# Waajiri walia gharama kubwa za kufanya biashara




Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Dk Aggrey Mlimuka. **Picha ya Maktaba**

**Mwandishi Wetu**, Mwananchi

Waajiri nchini wangependa kuongeza nafasi za kazi, lakini azma yao hiyo inaathiriwa na kile wanachoikiita gharama kubwa za kibiashara.

Gharama hizo zinachangiwa na masuala kadhaa ambayo kwa sasa Chama cha Waajiri wa Tanzania (ATE), kinasema kinaishawishi Serikali kuyashughulikia kwa kuwa yanaleta gharama za ziada kwa waajiri.

ATE ina wanachama takriban 1,300 na imekuwa na jukumu la kuhakikisha kunakuwapo mazingira mazuri ya kibiashara kwa waajiri tangu ilipoanzishwa mwaka 1960.

Inahakikisha sera na sheria zilizopo nchini zinatengeneza mazingira yatakayokuza biashara na kuleta ushindani. Wanachama wake wanatoka katika sekta mbalimbali zikiwamo kilimo, viwanda, wafanyabiashara, madini, benki na taasisi zingine za kifedha, wafanya biashara wa mafuta, watoa huduma mbalimbali pamoja na mashirika binafsi ya ulinzi.

Kwa sasa, ATE inashughulikia mambo kadhaa yafuatayo ili kuboresha mazingira ya kibiashara kwa waajiri nchini.

Tozo ya ujuzi na maendeleo (SDL)

Kwa miaka kadhaa, ATE imekuwa ikiishawishi Serikali kupunguza kiwango cha tozo hii ambacho mwanzoni kilikuwa asilimia sita ya mshahara ghafi wa mwajiri. Ushawishi huo ulisababisha kupunguzwa hadi asilimia tano iliyopo sasa.

Hata hivyo, ATE inaendelea na juhudi zake za kuishawishi Serikali kupunguza tozo hadi kufikia asilimia mbili, kiwango ambacho inaamini kitakuwa rahisi kutekelezeka na pia kuwavuta wafanya biashara wengi kurasimisha kazi zao na hivyo kuongeza wigo wa mapato ya kodi.

Kiwango cha asilimia tano kinaaminika kuwa cha juu kabisa siyo tu Afrika Mashariki bali pia duniani kote.

**Sheria ya fidia kwa wafanyakazi**

Sheria hii namba 20 ya mwaka 2008, ilianzisha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ambao unawataka waajiri kutoka sekta binafsi kuchangia asilimia moja ya malipo ya mishahara na asilimia 0.5 kwa waajiri wa sekta ya umma kuanzia mwaka wa fedha 2014/15.

Hata hivyo, malipo haya yanaonekana kama gharama za ziada kwa waajiri, kwani tayari wengi wao wanatoa huduma za bima za afya kwa wafanyakazi wao.

ATE inasema, mfuko huu umeondoa hata ile nafuu kidogo iliyotokana na kupunguzwa kwa tozo ya ujuzi na maendeleo (SDL).

Kanuni za ajira kwa wageni 2015

Kanuni hizi zinazosimamia ajira kwa watu wasio raia wa Tanzania zinaonekana kikwazo kimojawapo kwa waajiri, maana zinawabana wageni ambao ni nguvu kazi muhimu ikizingatiwa kwamba kuna changamoto za wafanyakazi wenye ujuzi.

ATE inasema waajiri wanataka sheria za kazi na uhamiaji zipunguze makali kwani zinaweza kujenga picha kwamba Tanzania haitaki wageni na hivyo kuwafukuza hata wawekezaji muhimu.

Inasema, kilicho muhimu kwa sasa ni kuwepo nguvu kazi imara katika kuendeleza nchi bila kujali mahali ilipotokea, huku Tanzania ikirekebisha mifumo yake ya elimu ili kuzalisha watu wanaokidhi mahitaji ya soko la ajira.

**Sheria ya ajira na mahusiano ya kazi 2004**

Waajiri wanataka marekebisho katika sheria hii ya ajira na uhusiano kazini, ili iweke wazi muda ambao mama mzazi anatakiwa kuondoka kazini kwa ajili ya kunyonyesha. Wakati sheria hii ikiwa wazi katika likizo za uzazi, bado haiko wazi kabisa kuhusu muda wa kunyonyesha.

Kwa mujibu wa ATE, suala la mama mzazi kuondoka kazini kwa ajili ya kunyonyesha linaathiri uzalishaji na wakati mwingine kuwafanya waajiri wafikirie mara mbili wanapomwajiri mwanamke.

**Mwelekeo mpya**

Pamoja na changamoto hizi zinazoendelea kuwasumbua waajiri, waajiri hao wana matumaini makubwa na Serikali mpya iliyopo madarakani chini ya kauli mbiu yake ya "Hapa Kazi Tu."

Hata hivyo, ATE inawataka waajiri kuungana kipindi hiki kuliko wakati mwingine wowote ili kuhakikisha madukuduku na mahitaji yao yanasikilizwa kwa wakati na Serikali iliyopo madarakani.

"Majadiliano ya wazi ni muhimu wakati waajiri tunashawishi mabadiliko. Kama kuna wakati ambao waajiri wangependa sauti zao zisikike kama muungurumo wa simba, basi ni sasa na siyo wakati mwingine," inasema sehemu ya taarifa ya ATE.

"Gharama za ufanyaji biashara zinatakiwa kupungua nchini na kurekebisha sheria hizi tata, huku waajiri wakishughulikia changamoto za kimiundombinu, tutaenda mbali zaidi na kuifanya Tanzania kuwa kivutio cha wawekezaji wa ndani na nje."

***Kwa maoni , tuma ujumbe mfupi kwa 0786240172. Maelezo yako yanathaminiwa sana na yakichapishwa katika gazeti utapewa muda wa maongezi wa Sh 30,000***

**SAUTI ZA WANANCHI**

**Dyoya Dyoya**

**Ili kuboresha mazingira ya biashara, nendeni tume ya mipango, SITRADE International walilofanya "harnessing the vision 2025", humo mikakati yote imeelezwa na hata mwelekeo wake umo. Ushauri wangu ni moja Katiba Mpya, mbili, umeme rahisi, tatu, miundombinu ya kiuchumi na nne miundo mbinu ya usafirishaji (barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, mawasiliano) mambo mengine yatakuwa yakifuata tena kwa rahisi na kasi usiyoitegemea.**

**Elineema Saro**

**Ili kuboresha mazingira ya sekta binafsi yafuatayo yafanyike; kwanza mfumo wa elimu ubadilike ili wahitimu waandaliwe kujiajiri na kuwa wajasiriamali badala ya kuwa wasakaji ajira. Pili Serikali izidishe upendeleo kwa wasambazaji, makandarasi, watoa huduma na washauri wa Kitanzania badala ya wageni. Tatu Serikali iongeze ujenzi wa miundombinu ya kijamii na kiuchumi ili kuiweka nchi kwenye nafasi ya kuwa sehemu ambayo uzalishaji ni wa gharama ndogo mfano usafiri, mawasiliano, afya, nishati na usalama. Serikali ipunguze urasimu kwenye huduma kama leseni, vibali na kodi**

**UKURASA HUU UMEDHAMINIWA NA**

BEST-Dialogue

Doing business, let's make it easy - and fair
Kufanya biashara kwa haki - bila vikwazo